# JE! UTAKWENDA MBINGUNI?

# Usidanganyike!!

Karibia jamii yote ya Kikristo wanatazamia kwenda mbinguni mara tu Kristo atakaporudi! Naam; ni karibia jamii zote za wanadamu kwa imani za dini na madhehebu yao wanatazamia kwenda mbinguni kwa Mungu, kwamba ni kwa njia ya kifo ama vyo vyote vile waaminivyo. Mawazo ya mioyo yao na mazungumzo ya vinywa vyao ni kuhusu shauku kubwa waliyonayo ya kuwa pale siku moja!

Nilimuuliza mtu fulani nikisema; *"Kwanini unataka kwenda mbinguni? Ni kitu gani kizuri huko kisichopatikana duniani?"* Mtu huyo alinijibu kwamba; *"Kwa sababu mbinguni ni mahali patukufu palipojawa na amani na furaha. Pia Mungu yupo pale daima; kwa hivyo mahitaji yako na msaada wo wote utakaouhitaji unapatikana mara moja kwa urahisi na uhakika".* Aliielezea dunia kama mahali palipojaa kila aina ya matatizo yatukabiliyo katika maisha. Basi nikamuuliza zaidi; *"Ni kitu gani kimepafanya huko mbinguni kuwa mahali pazuri namna hiyo, huku duniani kukijawa na maovu? Hakuna lo lote liwezalokufanywa ili dunia iwe mahali pa amani kama mbinguni na kufaa kwa maisha ya umilele?"* Alinijibu kwa haraka akisema; *"Hapana! Haiwezekani kabisa. Hata Mungu mwenyewe anajua ya kuwa dunia imeharibika kwa uovu kiasi cha kutorekebishika. Ndiyo sababu Kristo atakuja kutuhamisha hapa na kutupeleka mbinguni; kisha aiteketeze dunia kwa moto".*

Basi nikuulize wewe mpendwa uusomaye ujumbe huu. Je! wewe pia una mawazo na imani kama ya huyo jamaa tuliyehojiana naye kuhusu habari hizi? Kama jibu lako ni ndiyo; basi jiandae kushitushwa na ukweli wa kushangaza unaokwenda kufunuliwa kwako na Mungu muumba wako kupitia jarida hili! Basi je! Mungu anasema ni kitu gani kitafanyika mara baada ya kurudi kwa Yesu Kristo?

## MBINGU ZA MBINGU NI ZA MUNGU

Mungu aliyeumba vitu vyote ukiwemo na wewe anasema; ***"Mbingu ni kiti changu cha enzi, Na nchi*** *{dunia}* ***ni pa kuwekea miguu yangu…Matendo 7:49.*** Mungu anaonesha dhahiri hapa kwamba; mbinguni ni makao yake makuu hivi sasa. Na mwonekano wake huko ni kama hivi; ***"Kichwa chake na nywele zake*** *{ni}* ***nyeupe kama sufu nyeupe, kama theluji; na macho yake kama mwali wa moto; na miguu yake kama shaba iliyosuguliwa sana…na sauti yake kama sauti ya maji mengi…na uso wake kama jua liking'aa kwa nguvu zake" Ufunuo 1:14-16;*** *soma pia* **Daniel 7:9.**

Paulo anauelezea huo utukufu kwa namna ya pekee akisema; ***"…Yeye** {Mungu}**…amekaa katika nuru isiyoweza kukaribiwa; wala hakuna mwanadamu aliyemwona, wala awezaye kumwona…" 1 Timotheo 6:16.*** Basi ni hii asili ya utukufu ndiyo inayoifanya mbingu kuwa mahali pazuri ajabu! Daudi anashuhudia huku akisifu kwa mshangao akisema; ***"Mbingu zauhubiri utukufu wa Mungu, Na anga laitangaza kazi ya mikono yake" Zaburi 19:1.*** Umewahi kujiuliza ni kwanini Mungu pamoja na mbingu yake ni tukufu kiasi cha wewe kutamani kuwepo pale?

## UTUKUFU NI MATUNDA YA MAISHA YA MUNGU

Kila andiko linalomzungumzia Mungu, linamwelezea *{kumwonesha ama kumfafanua}* kuwa ni Mtukufu, Mtakatifu, mwenye haki, wa kweli na mengine mengi yanayoonesha ukamilifu. Na kwa vile Mungu alimuumba mtu ili mtu huyo awe kama yeye alivyo; amejifunua na kujitambulisha yeye, maisha yake pamoja na mipango yake ya uumbaji kwa manabii na mitume ili hao wawafundishe watu wote waliosalia habari hizo. Maana imeandikwa; ***"Baada ya mambo haya nitarejea, Nami nitaijenga tena nyumba ya Daudi iliyoanguka…Ili wanadamu waliosalia wamtafute Bwana Na mataifa yote ambao jina langu limetajwa kwao; Asema Bwana…" Matendo 15:16-18.***

Basi hao manabii na mitume wakifanya kazi waliyoagizwa wanasema; ***"…Sisi nasi tu wanadamu hali moja na ninyi; twawahubiri habari njema, ili mgeuke*** *{mtubu}* ***na kuyaacha mambo haya ya ubatili na kumwelekea Mungu aliye hai, aliyeumba mbingu na nchi na bahari na vitu vyote vilivyomo" Matendo 14:15.***

Ni kitu gani basi tunachomaanisha hapa? Ni kwamba; maandiko ya Biblia ni ufafanuzi wa Mungu kwa wanadamu uhusuo hayo maisha ya Mungu ya utukufu *{tafadhali soma maandiko haya katika biblia yako.* ***Zaburi 19:7-8; 119:9-10, 130, 114, 137-138, 142, 165, 172****}*. Naam; hii ndiyo sababu Paulo anashuhudia akisema; ***"Kila andiko, lenye pumzi ya Mungu*** *{ama litokalo kwa Mungu}****, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki; ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema" 2 Timotheo 3:16-17.***

Hivyo basi wapendwa; ni kwa kuishi kwa yale ayafafanuayo Mungu katika biblia ndiko kunakofanyiza *{ama kupeleekea kuwepo kwa}* ulimwengu mtukufu! Maana kama ilivyoandikwa; ***"Maagizo ya BWANA ni ya adili, Huufurahisha moyo. Amri za BWANA ni safi, Huyatia macho nuru" Zaburi 19:8.*** Tena; ***"Wana amani nyingi waipendao sheria yako, Wala hawana la kuwakwaza" Zaburi 119:165.*** Naam; kuishi kwa haya maagizo ya Mungu ndiko kunaifanya mbingu kuwa na uzuri wa ajabu, amani na furaha kuu; naam, kuwa maridhawa kiasi cha kukufanya wewe usikiapo habari zake, utamani kwenda kuishi pale! Lakini hata ingawa ni pazuri hivyo; je! Mungu ameahidi kukupeleka huko?

## MUNGU AMEIUMBA DUNIA KUWA SEHEMU YA UFALME WAKE

Rafiki; je! unafahamu ya kuwa kuna wakati ambapo hii Dunia ilikuwa sehemu ya Ufalme mtukufu wa Mungu, ukiongozwa kwa mujibu wa sheria takatifu za Mungu? Pengine hujawahi kabisa kusikia habari hizi; na hii ni kwa mara ya kwanza unasikia! Ndiyo sababu tulikwambia awali kwamba, utegemee kushitushwa na ukweli wa kushangaza ndani ya biblia kupitia jarida hili!

Wakati Mungu alipoiumba Dunia hii; aliiumba yenye kuvutia, nzuri sana, yenye kutamanika kiasi kwamba, malaika walipoishuhudia ilivyoumbwa hawakuficha hisia zao kama ilivyoandikwa; ***"Hapo nyota*** *{yaani, malaika; soma Ufunuo 1:20}* ***za asubuhi zilipoimba pamoja, Na wana wote wa Mungu walipopiga kelele kwa furaha…" Ayubu 38:7.***

Akithibitisha hali hiyo ya urembo wa ajabu ambao Dunia iliumbwa kwao, Isaya anasema; ***"Maana BWANA, aliyeziumba mbingu, asema hivi; Yeye ni Mungu; ndiye aliyeiumba dunia na kuifanya; ndiye aliyeifanya imara; hakuiumba ukiwa…" Isaya 45:18.*** Naam; hii dunia ilisheheni uzuri wote; ikiwa ni Ikulu ndogo ya Mungu, ikiongozwa na viumbe wa roho *{malaika}* kwa sheria za Mungu. Lakini baadaye hao viumbe *{malaika}* watakatifu waliasi ***{soma Ezekieli 28:15-16}.*** Na ndipo baada ya uasi huo wa malaika *{soma pia Yuda 1:6; 2 Petro 2:4}*; ***"…nchi*** *{dunia}* ***ilikuwa ukiwa, tena utupu, na giza lilikuwa juu ya uso wa vilindi vya maji…" Mwanzo 1:2.*** *{Kwa maelezo ya kina zaidi kuhusu mada hii; agiza ujumbe wetu usemao,* ***"SHETANI NI NANI?"****, na utatumiwa bure ujumbe huo}.*

## MPANGO WA MUNGU WA KUUREJESHA UFALME WAKE DUNIANI

Kwa vile mpango wa Mungu hauwezi kuzuiliwa na awaye yote; basi alianza mchakato wa kuurejesha tena Ufalme wake hapa duniani kwa kuikarabati tena dunia kwa muda wa siku sita ***{soma Mwanzo 1:3-27}.*** Na hizi siku sita za juma ni unabii unaoeleza kipindi atakachochukua Mungu mpaka kuukamilisha huo urejeshwaji wa ufalme huo kikamilifu. Baada ya huo ukarabati wa dunia kwa siku sita; dunia ilikuwa nzuri sana, yenye kupendeza ***{soma Mwanzo 1:31}.***

Basi kwa vile sasa dunia imerejeshwa katika hali nzuri; ni nani ambaye Mungu amtumie kuitawala? Naam; ***"Mungu akasema, Na tumfanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu; wakatawale…juu ya nchi" Mwanzo 1:26.*** Kwa hivyo rafiki; ni jambo la pekee sana kwamba wewe na mimi tuliumbwa kwa kusudi la kuitawala dunia; na kwa kupitia kwetu, Mungu aurejeshe tena ufalme wake hapa!

Lakini kama tulivyokwishaona awali; ufalme wa Mungu duniani ulikuwa ufalme mtukufu wa kiroho, ukitawaliwa na viumbe watukufu wa roho kwa mujibu wa sheria takatifu za Mungu. Halafu Mungu kupitia kwa mtume Paulo anatuambia; ***"…ya kuwa nyama na damu***

*{yaani mwili huu tulionao sasa}* ***haziwezi kuurithi ufalme wa Mungu…" 1 Wakorintho 15:50.*** Inakuwaje basi kwamba Mungu anakusudia kufanya jambo lisilowezekana kwa mwanadamu wa mwili wa nyama na damu kuurithi na kuumiliki ufalme wake?

## NI SHARTI MTU APEWE MWILI WA ROHO KWANZA

Kama tulivyokwishasema; mpango wa urejeshwaji wa ufalme wa Mungu duniani unachukua kipindi cha siku saba za juma. Kwa maana kwamba; siku moja inamaanisha ama kuwakilisha miaka elfu moja; na hivyo kufanya siku saba kumaanisha miaka elfu saba ***{soma 2 Petro 3:8; Zaburi 90:4}.*** Katika kipindi cha miaka elfu sita; mwanadamu amepewa nafasi ya kuzaliana na kuijaza dunia, huku akijifunza tabia takatifu ya Mungu kwa njia ya sheria takatifu za Mungu *{mfumo pekee wa maisha unaopafanya mbinguni kuwa mahali pazuri jinsi palivyo}.* Kisha Mungu anaeleza wazi kwamba, miaka elfu moja ya mwisho *{inayoashiriwa na siku ya saba ya juma, yaani sabato}* inayokamilisha miaka elfu saba, itakuwa ya Ufalme wa Mungu kurejeshwa kikamilifu duniani; naam, ni Sabato ya Bwana.

Hata hivyo; Adamu alidanganywa na Shetani, naye akawarithisha uzao wake *{yaani wanadamu wote}* udanganyifu huo! Na kwa sababu hiyo; wanadamu wakapuuza na kutupilia mbali *{hawajui kabisa}* sababu na kusudi la kuumbwa kwao! Lakini pamoja na hayo; ***"…kila kazi aifanyayo Mungu itadumu milele; haiwezekani kuizidisha kitu, wala kuipunguza kitu…" Mhubiri 3:14;*** *soma pia* ***Isaya 46:10.***

Basi kwa vile dhumuni la kuumbwa kwetu ni ili Mungu atutumie kuurejesha na kuutawala Ufalme wake hapa Duniani; huku pia mwanadamu amedanganyika na kuupuuza mpango huo na hata kutoufahamu kabisa; Mungu alimtuma Yesu Kristo na Ujumbe wa ukumbusho wa jambo hili.

## INJILI NI HABARI NJEMA ZA UREJESHWAJI WA UFALME WA MUNGU DUNIANI

Kristo alianza kuuwasilisha ujumbe wake kwa kusema; ***"Wakati umetimia, na ufalme wa Mungu umekaribia; tubuni, na kuiamini Injili" Marko 1:15.*** Wakati upi? Kipindi cha miaka elfu saba kinakaribia kuisha. Hii ndiyo sababu Ufalme umekaribia. Lakini anawaambia watu kwamba wanahitaji kubadilika *{kutubu/kugeuka}* kutoka katika mfumo wa maisha ya Kishetani waishio kwao hivi sasa. Maana ni kwa kuzikataa sheria takatifu za Mungu ndiyo sababu dunia imetiwa unajisi na kuwa mahali pa vurugu, kama ilivyoandikwa; ***"…dunia imetiwa unajisi kwa watu wanaoikaa; kwa maana wameziasi sheria, wameibadili amri, wamelivunja agano la milele. Ndiyo sababu laana imeila dunia hii, na hao wanaoikaa wameonekana kuwa na hatia…" Isaya 24:5-6.***

Basi kwa wale wanaomkubali Kristo na ujumbe wake wanapokea roho takatifu ndani yao, na kwa msaada wa roho hiyo wanaanza kujifunza na kupigania kuishi kwa sheria hizo takatifu za Mungu. Maana Kristo anaagiza akisema; ***“Mkinipenda, mtazishika amri zangu” Yohana 14:15.*** Amri zipi? Amri za Kristo ni amri kumi za Mungu ***{soma Yohana 12:49-50; Mathayo 19:16-19; Kutoka 20:3-17}.*** Watakapofuzu kujifunza maisha hayo ya Mungu; ni kitu gani kitakuwa thawabu yao pindi Kristo atakaporejea?

## WATAKATIFU KUITAWALA DUNIA HII

Kristo aliahidi akisema; ***“Yeye ashindaye*** *{katika kujifunza maisha ya Mungu}****, nitampa kuketi pamoja nami katika kiti changu cha enzi…” Ufunuo 3:21.*** Haya yatafanyika wapi? Je! ni juu mbinguni aliko Kristo hivi sasa? Ingawa Kristo aliahidi kurudi tena ili atuchukue tukae mahali atakapokuwa yeye; lakini kamwe hakusema ni mbinguni ***{soma Yohana 14:1-3}.*** Sasa basi; je! ni wapi kiti chake cha enzi kitakapokuwa?

***“Kwa sababu Bwana mwenyewe atashuka kutoka mbinguni pamoja na mwaliko, na sauti ya malaika mkuu, na parapanda ya Mungu*** *{soma pia 1 Wakorintho 15:2};* ***nao waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza. Kisha sisi tulio hai, tuliosalia, tutanyakuliwa pamoja nao katika mawingu, ili tumlaki*** *{yaani tumpokee}* ***Bwana hewani; na hivyo tutakuwa pamoja na Bwana milele” 1 Wathesalonike 4:16-17.***

Basi watu kwa kutoyaelewa maandiko haya; wanaingiza dhana zao kwamba tutamlaki Bwana na kurudi naye mbinguni, huku wengine wakidai kuwa tutaishi naye miaka saba hapo hewani tulipomlaki! Lakini kamwe Biblia haijasema mambo haya mahali po pote pale! Sikilizeni tafadhali.

Kwanza kabisa; pindi watu waliokufa katika Kristo *{katika mafunzo ya maisha ya Mungu}* watakapofufuliwa; na kunyakuliwa pamoja na wale watakaokutwa hai; watabadilishwa kutoka katika mwili huu wa nyama na damu na kupewa mwili wa roho na hivyo kutimiza kusudi la Mungu la *“kumfanya mtu aliye kama yeye {****Mwanzo 1:26****}”*. Kisha; baada ya kufanywa kuwa viumbe wa roho; kutoka hapo hewani wataelekea moja kwa moja juu ya mlima wa Mizeituni *{ama mlima Sayuni}* uliopo mashariki ya kati, katika nchi ya Israeli, kwenye mji wa Yerusalemu hapa Duniani. Akiuzungumzia ujio huo wa Kristo, nabii zekaria anasema; ***“Na siku hiyo miguu yake*** *{Bwana/Kristo}* ***itasimama juu ya mlima wa Mizeituni, unaoelekea Yerusalemu upande wa mashariki, nao mlima wa Mizeituni utapasuka katikati yake…” Zekaria 14:4.***

Basi je! ni Kristo peke yake ndiye atakayeshuka hapo juu ya mlima wa Mizeituni? Naam; Zekaria anasema; ***“…na BWANA Mungu wangu*** *{Yesu Kristo},* ***atakuja, na watakatifu wote*** *{waliobadilishwa kuwa viumbe wa roho katika kumlaki}* ***pamoja naye” Zekaria 14:5.*** Kisha ni kitu gani kitafuata? Je! Bwana atarudi mbinguni alikotoka pamoja na hao watakatifu? Zekaria

anasema; ***"Naye BWANA atakuwa Mfalme juu ya nchi yote*** *{sio mbingu, tafadhalini}****; siku hiyo BWANA atakuwa mmoja, na jina lake moja" Zekaria 14:9.***

Basi huo utakuwa ni mwanzo wa utawala wa miaka elfu moja ya Kristo pamoja na watakatifu wake duniani *{yaani Milenia}*. Maana Yohana pia anasema; ***"Kisha nikaona viti vya enzi, wakaketi juu yake, nao wakapewa hukumu; nami nikaona roho zao waliokatwa vichwa kwa ajili ya ushuhuda wa Yesu na kwa ajili ya neno la Mungu…nao wakawa hai*** *{wakafufuka katika ujio wa Kristo wakati wa parapanda ya Mungu}****, wakatawala pamoja na Kristo miaka elfu" Ufunuo 20:4.*** Mwenye ufahamu na afahamu tafadhalini. Watakatifu watapewa hukumu kutimiza ahadi ya Yesu aliyoahidi akisema; ***"Na yeye ashindaye, na kuyatunza matendo yangu hata mwisho*** *{kwa kuishi kwa mafunzo ya Kristo; yaani sheria za Mungu}****, nitampa mamlaka juu ya mataifa*** *{juu ya wanadamu waliosalia wenye mwili wa nyama na damu}****, naye atawachunga kwa fimbo ya chuma…" Ufunuo 2:26-27.***

Basi je! hayo yatafanyika wapi? Yohana anasema; ***"ukawafanya*** *{hao walioshinda}* ***kuwa ufalme na makuhani kwa Mungu wetu; nao wanamiliki*** *{wanatawala}* ***juu ya nchi*** *{sio mbinguni, tafadhalini}****" Ufunuo 5:10.***

## DUNIA KURUDISHWA KATIKA HALI YAKE YA AWALI

Mara tu watakatifu watakaposhika hatamu *{yaani kuchukua na kushika uongozi};* watairekebisha dunia kwa kuwafundisha watu sheria za Mungu. Kumbukeni katika ***Isaya 24:4-6*** tuliona kwamba dunia imetiwa unajisi kwa watu kukataa sheria za Mungu ambazo pekee ndizo ziwezazo kuifanya kuwa safi. Basi Ufalme wa Mungu utakaposimamishwa; watoto wa Mungu waliofanywa kuwa viumbe wa roho *{yaani hao watakatifu},* wataitawala dunia kwa mujibu wa sheria za Mungu. Na hii itakuwa ni mara baada ya Ibilisi Shetani ambaye hivi sasa anaudanganya ulimwengu wote kuwa amekamatwa na kutiwa kifungoni asipate nafasi ya kuwadanganya watu kwa kipindi hicho ***{soma Ufunuo 12:9; 20:1-3}.***

Basi kuanzia wakati huo; ***"…waokozi*** *{yaani watakatifu}* ***watakwea juu ya mlima Sayuni*** *{ama mlima wa Mizeituni}* ***ili kuuhukumu mlima wa Esau; nao huo ufalme utakuwa ni mali*** *{ama milki}* ***ya BWANA" Obadia 1:21.*** Na kwa kuwa Shetani ameondolewa asiwadanganye watu; basi, ***"Miisho yote ya dunia itakumbuka, Na watu watamrejea BWANA; Jamaa zote za mataifa watamsujudia. Maana ufalme una*** *{ama ni wa}* ***BWANA, naye ndiye awatawalaye mataifa" Zaburi 22:27-28.***

Naam; machafuko na vurugu zote zikufanyazo kutamani kuihama dunia na kwenda mbinguni zitakomeshwa kabisa; maana mioyo ya uasi na ukaidi itaondolewa na mahali pake kuchukuliwa na mioyo ya uchaji Mungu. Maana; ***"…mataifa mengi watakwenda na kusema, Njoni, twende juu mlimani kwa BWANA, nyumbani kwa Mungu wa Yakobo, naye atatufundisha njia zake*** *{jinsi ya kuishi},* ***nasi tutakwenda katika mapito yake, maana katika***

***Sayuni itatoka sheria, na neno la BWANA katika Yerusalemu*** *{mji Mkuu wa Ufalme wa Mungu duniani; Yeremia 3:17}.* ***Naye atafanya hukumu katika mataifa mengi, atawakemea watu wa kabila nyingi; nao watafua panga zao ziwe majembe, na mikuki yao iwe miundu*** *{yaani zana za vita zibadilishwe kuwa zana za kilimo};* ***taifa halitainua upanga juu ya taifa lingine, wala hawatajifunza vita tena kamwe" Isaya 2:3-4;*** *soma pia* ***Zaburi 2:8-9.*** Naam; ***"Hawatadhuru wala hawataharibu katika mlima*** *{ufalme}* ***wangu wote mtakatifu; maana dunia itajawa na kumjua BWANA, kama vile maji yanavyoifunika bahari" Isaya 11:9.***

Uharibifu wa mazingira unaopeleekea kutositawi kwa mazao ya chakula na mimea kwa ujumla, na pia kupeleekea magonjwa utakomeshwa! Naam; ***"Nyika na mahali palipo ukiwa patafurahi; jangwa litashangilia na kuchanua maua kama waridi…Ndipo macho ya vipofu yatafumbuliwa, na masikio ya viziwi yatazibuliwa. Ndipo mtu aliye kilema ataruka-ruka kama kulungu, na ulimi wake aliye bubu utaimba…"*** *Tafadhali soma* ***Isaya 35:1-7; 32:1-4.***

Naam; Dunia itakuwa Ufalme Mtukufu wa mbinguni kwa sababu sheria za haki za Mungu ndizo zitakuwa kipimo cha hukumu, kutimiza sala ya Kristo kwa Baba kwamba, ***"Mapenzi yako yatimizwe, hapa duniani kama huko mbinguni" Mathayo 6:10.*** Na hivyo kama tulivyokwishasema; Dunia itakuwa mahali pazuri pa kuishi palipojaa utulivu, amani na furaha kwa sababu, ***"…dunia itajawa na kumjua BWANA, kama vile maji yanavyoifunika bahari" Isaya 11:9.***

Basi wapendwa; hiki ndicho wanachokingojea kwa shauku nyingi walio Wakristo wa kweli na waabuduo halisi wa Mungu. Hawatahamishwa kwenda mbinguni, na badala yeke, Ufalme wa mbinguni utawajia hapa hapa duniani ili kutimiza kile Kristo alichowaahidia akisema; ***"Heri wenye upole; Maana hao watairithi nchi" Mathayo 5:5*** *{soma pia Danieli 2:44; 7:13-14,18,27; na kwa maelezo ya kina zaidi kuhusu mada hii, agiza ujumbe wetu usemao, "UFALME WA MBINGUNI", ama usemao, "ULIMWENGU MARIDHAWA UJAO", ili ujifunze zaidi; nasi tutakutumia bure masomo hayo}.*

Wapendwa; hii ndiyo Injili ya kweli iliyohubiriwa tangu zamani na Manabii, Yesu Kristo, pamoja na Mitume wake; ambayo nasi leo Kanisa la Mungu tunaihubiri kwenu kama tulivyoagizwa ***{soma Mathayo 28:19-20}.*** Basi tunahitimisha kwa maneno ya Kristo tukisema; ***"Wakati umetimia, na ufalme wa Mungu umekaribia; tubuni*** *{geukeni},* ***na kuiamini Injili" Marko 1:15.*** Uko tayari kwa hili? Na je! utapenda kujifunza zaidi ukweli halisi wa Biblia ili kuepukana na waalimu na manabii wa uongo waliojaa duniani huku wakiwaelekeza watu katika ibada za bure machoni pa Mungu? ***{soma Marko7:6-7; Yohana 8:31-32}.*** Wasiliana nasi kwa anuani zifuatazo:-

**KANISA LA MUNGU – TANZANIA**

**Mwanza –** Simu; +255 753 359 179, +255 688 359 179 & +255 655 659 179.

WhatsApp; +255 655 659 179.

Barua pepe; Ukweliwabiblia @yahoo.com.sg

**Arusha –** Simu; +255 754 028 574 & +255 782 422 216.

**Dar Es Salaam –** Simu; +255 762 055 056 & +255 672 611 204.

**KANISA LA MUNGU – KENYA**

**Nairobi –** Simu; +254 739 434 639.

Barua pepe; endcog@gmail.com

Wavuti;www.endtimecog.org

**KANISA LA MUNGU – UGANDA**

**Kampala –** Simu; +256 754 167 854